**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 24 Juni, 2015**

*(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani taarifa ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Afya wa Wilaya, na taarifa ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Miundombinu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**KAULI YA SERIKALI**

**Kuanzishwa kwa Mfuko wa Afya wa Wilaya na Mfuko wa Miundombinu**

**Mhe. Spika:** Hivi Kamati hawakutayarisha maoni yoyote ya maandiko? Ziko Kamati mbili hizi. Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Awali ya yote naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini naomba tu labda tujikumbushe. Kwenye Kanuni zetu kwenye Kauli za Serikali kamati inakuwa haina taarifa, kwa sababu hii ni kauli ya Serikali, labda makatibu watusaidie.

**Mhe. Spika:** Hii si Kauli ya Serikali, hii ni Taarifa ya Serikali, na tukiangalia Ibara ya 44 inazungumzia kwamba hebu twende kwenye Ibara ya 44.

> 44(1)"Waziri anaweza kuwasilisha taarifa ya Serikali katika Baraza kuhusiana na jambo ambalo serikali inahitaji kuliarifu Baraza".
>
> 44(3)Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na Kamati atapewa nafasi ya kutoa maoni kwa niaba ya Kamati kuhusiana na taarifa hiyo ya Serikali".

Sasa kama kuna maandiko inabidi hati yake iwekwe mezani, lakini kama atatoa hivi hivi tu sasa hiyo ndio anaweza akatoa maoni moja kwa moja bila ya kuweka hati mezani.

Sasa ndio nikauliza hivi Kamati walitayarisha maoni yoyote yaliyoandikwa kama Kamati. Kwa sababu hii kwamba Mwenyekiti wa Kamati au Mjumbe aliyeidhinishwa na Kamati ni kama utaratibu wa kawaida.

Sasa na hapa kutakuwa na Kamati mbili kwa kuwa hizi taarifa ni mbili; moja ya Miundombinu na moja inahusu Mfuko wa Afya, kutakuwa na Kamati ya Ustawi wa Jamii na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Kwa sababu ndio inayohusu mambo ya Miundombinu.

Sasa angalau nijue kuna maandiko yaliyotayarishwa Kamati ya Ustawi wa Jamii. Tuanze na Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuna Mjumbe yeyote, hakuna. Basi itakuwa ni maoni yaliyokuwa hayakuandikwa. Tutaruhusu yatolewe hivi hivi tu. Kamati ya Miundombinu Mwenyekiti.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba muongozo wako kabla sijaelekea katika haya masuala yenyewe.

Pamoja na taarifa yako Mhe. Spika, kwamba hii ni Taarifa ya Serikali imetumia Kifungu cha 44 cha Kanuni, lakini hapa katika *order paper* hii ni Kauli ya Serikali. Sasa ningeliomba muongozo wako tunajadili taarifa ya Serikali au tunajadili Kauli ya Serikali. Naomba muongozo wako Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Niitake Serikali wanakusudia iweje, kwa sababu Kauli ya Serikali haijadiliwi huulizwa maswali, taarifa ya serikali inajadiliwa. Sasa mnakusudia ifanyweje, hebu niambieni.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, haya ambayo aliyoyafanya Mhe. Waziri wa Fedha ni kufuata masharti ya Sheria Nam. 12 ya 2005 ambayo ni sheria inayoelekeza kama pale ambapo Mhe. Waziri anayehusika na fedha ataanzisha mfuko wowote ili taarifa yake ya uanzishwaji wa ule mfuko ni lazima iletwe kwenye Baraza la Wawakilishi.

Sasa hichi ambacho kinafanywa leo ni kuleta ile taarifa ya serikali kuhusiana na kuanzishwa na ule mfuko wenyewe nayo ni mifuko miwili. Mfuko wa Miundombinu na Mfuko ule wa Kuanzishwa Mfuko wa Afya ya Wilaya.

Kwa hivyo, hii ni taarifa Mhe. Spika, ya serikali inayoletwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 12 ya 2005 chini ya Kifungu cha 11 cha sheria hiyo.

**Mhe. Spika:** Kwa hiyo, kama ni taarifa ya Serikali utaratibu wake ijadiliwe, na kwa hii *order paper* kwa maana hiyo itabidi tunairekebisha isiwe Kauli ya Serikali, ila ni Taarifa ya Serikali.

Sasa kama Wenyeviti wale wanaohusika na maeneo haya watakuwa wamekubaliana na Wajumbe wenzao, kwamba Mwenyekiti atakalotoa ndio kwa niaba ya Kamati basi atatoa kwa utaratibu huu wa kawaida, tukubaliane hivyo labda.

Sasa Wenyeviti wote wawili hao wajitayarishe kutafuta maneno ya kusema kwa niaba ya Kamati. Kwa upande wa Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii lakini pia kwa upande wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Baada ya hapo sasa namuomba Mhe. Waziri wa Fedha kuja kutoa hiyo taarifa.

## TAARIFA YA SERIKALI

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nitimize wajibu wangu wa kisheria chini ya kifungu cha 11cha Sheria ya Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2005 kilichompa uwezo waziri mwenye dhamana ya fedha kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya matumizi maalum.

Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo mafupi juu ya sababu na madhumuni ya uanzishwaji wa Mfuko wa Huduma za Afya Wilayani katika mwaka wa bajeti inayomalizia 2014/15.

Serikali ilifanya tathmini juu ya miradi tofauti na kugundua baadhi ya miradi haikidhi vigezo vya kisheria ya fedha za umma na kuamua kuiondoa katika orodha ya miradi ya maendeleo ya serikali. Kutokana na hali hiyo serikali imeona kuna haja ya kuanzisha Mfuko Maalum wa Huduma za Afya wilayani kufuatia makubaliano baina ya serikali na wahisani wa maendeleo yaliyosainiwa mwezi wa Mei, 2012 kwa madhumuni ya kusaidia huduma za afya wilayani.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kifungu cha 11 cha Sheria ya Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2005 kinamtaka Waziri wa fedha kuwasilisha mbele ya Baraza lako hati ya kuanzishwa mfuko huo kabla ya kuanza kutumika kwake. Mhe. Spika, hati ya kuanzishwa kwa mfuko huo ina sehemu kuu sita:-

### Sehemu ya Kwanza

Utangulizi wa chanzo cha kuanzishwa kwa mfuko huo.

### Sehemu ya Pili

Madhumuni na malengo ya Mfuko.

**Sehemu ya Tatu**

Msimamizi wa Mfuko huo; ambapo Katibu Mkuu Wizara ya Afya atakuwa msimamizi na Afisa mas-uli wa mfuko.

**Sehemu ya Nne**

Uanzishwaji wa Kamati ya Uendeshaji wa Mfuko huo ambapo Wajumbe watatoka serikalini pamoja na wahisani wa maendeleo.

**Sehemu ya Tano**

Vyanzo na Utoaji wa fedha katika mfuko huo. Ambapo Serikali pamoja na wahisani wa maendeleo watachangia fedha zao katika akaunti maalum ya pamoja ya mfuko huo.

**Sehemu ya Sita**

Masharti ya Ukaguzi wa Mfuko huo. Ambapo taratibu za ukaguzi zitatumika za taasisi za kimataifa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ya uanzishwaji wa hati ya uanzishwaji wa mfuko huo, kwa idhini yako sasa naomba kuwasilisha taarifa ya uanzishwaji wa Mfuko wa Huduma za Afya Wilayani.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

**Mhe. Spika:** Hapa zimewekwa kwamba mifuko yote miwili taarifa yake itawasilishwa kwa pamoja. Basi endelea halafu tutaita kwa mtiririko wa mmoja baada ya mwengine. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii halafu na Mwenyekiti makini sana wa Mawasiliano na Ujenzi. (*Makofi*).

**MUONGOZO**

**Mhe. Hamza Hasssan Juma:** Mhe. Spika, nilikuwa naomba muongozo wako.
Mhe. Waziri anasoma ripoti yake sina uhakika kama labda mimi yangu sijui nimeipoteza au kama kuna *document* yoyote ambayo tuliyosambaziwa ili tukaweza kupata kuichangia vizuri, na ndio maana nikasema sina uhakika, inawezekana pengine zimesambazwa lakini mimi sijaiona yangu, na wenzangu nilikuwa najaribu kuwauliza na wao hawajaiona.

Sasa kwa sababu Mhe. Spika, tunajadili kitu ambacho tunataka kukiweka kisheria lazima tupate yale maeneo ambayo tutataka kushauri. Jengine ambalo limependekezwa tunaweza tukasema hili litoke. Lakini sasa *document* mimi naona sina, sasa mimi nafikiri Mhe. Waziri sio tatizo, muache aendelee amalize kusoma, lakini *documents* ziwe *circulated* kwa Wajumbe ili tupate na sisi kuzipitia basi tupate kuchangia vizuri katika hii hoja ya Mhe. Waziri. Kimsingi hoja tumeshaikubali, lakini ni vizuri tukapata *document* ambayo tukajaribu kujadili vile vipengele ambavyo walivyovipendekeza.

Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Nafikiri ni jambo la maana, na sina hakika kama uwasilishaji uliowasilisha ni kamili au vipi maana naona umewasilisha kwa ufupi sana. Maana umetaja kuna maeneo sita, hiyo taarifa yenyewe maneneo mangapi?

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Naam.

**Mhe. Spika:** Hiyo taarifa yenyewe ina maeneo mangapi? Umesema umetaja kitu hapa.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Hii ya kwanza ina maeneo sita.

**Mhe. Spika:**Sasa maeneo sita hayo inavyoonekana Wajumbe wanataka wayaone ni lipi na lipi na linaelezea nini ndio wakaomba hizi *documents* zingesambazwa humu ndani ili wakaweza kupitia pitia. Sijui kama Makatibu mlipewa *documents* mka-*reproduce* hakuna kitu mlichoki-*reproduce* Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, hayo ambayo ameyasema Mhe. Hamza Hassan Juma ni sahihi, na yale ambayo wewe Mhe. Spika, kama ambavyo umeyatolea ufafanuzi ni sahihi.

Ni kweli inabidi Wajumbe wapate na waone kile ambacho kinawasilishwa na Mhe. Waziri wa Fedha wakichangie, na ikibidi kama kuna masahihisho yafanywe ili sasa itoke ile *order* ambayo sasa itakuwa imeridhiwa na Baraza na itayokwenda kutangazwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Taarifa hizo ziko kwenye meza ya Katibu nadhani wanamalizia tu kuzitoa *photocopy* muda tu ulikuwa mdogo zilipowasilishwa, lakini zipo zimeshawasilishwa zinatolewa *photocopy* labda pale ambapo Mhe. Waziri atamaliza, *of course* na Kamati nayo pia ina nafasi yake, labda hapo sasa baadae itabidi tutafute muongozo mwengine ili sasa Kamati na Wajumbe wapewe nafasi ili sasa waweze kuja kuchangia taarifa hizi.

**Mhe. Spika:** Hebu nambie Mhe. Waziri hii taarifa ya Mfuko wa Wilaya ina urefu gani, inaweza kuchukua muda gani kuisoma kama ilivyo.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Hii ya Miundombinu au ya Wilaya?

**Mhe. Spika:** Ya Wilaya.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Ya Wilaya nimeshamaliza kusoma. Ya Wilaya imekwisha, hii ina vifungu sita tu. Sasa hivi nataka kusoma Miundombinu. Au nivirudie vifungu wavisikie kwa utaratibu?

**Mhe. Spika:** Hebu virudie ili wafuatilie kwa makini sana. Haya sasa napewa taarifa hapa kwamba hii ya Mfuko wa Wilaya ilikwishatolewa huko nyuma sina hakika kama Wajumbe mlikwishaipata. Hii ya Miundombinu kwa kweli bado haijatayarishwa, sasa tunafanyaje?

Labda nisikie Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi anasemaje.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, ni sawa na maelezo ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu amekwishayazungumza sasa hivi, na kwa kukubaliana na hoja ambayo Mwenyekiti wa Wenyeviti pale amekwishazungumza juu ya suala la hizi *documents*, lakini hata sisi kama Kamati ili tuweze kuja kutoa maoni yetu tunaomba na angalau japo dakika tano Mhe. Spika, ili tuweze kupitia hiyo ripoti yenyewe ya huo mfuko, halafu tuweze kuja kutoa hayo maoni yetu hapa katika hichi chombo kinachohusika.

Kwa msingi huo naomba Mhe. Spika, tusitishe Baraza lako kwa muda mfupi tukafanye hayo, baadae tuweze kurejea tena tuendelee na utaratibu wetu kama ambavyo tunajipangia. Naomba kuwasilisha Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Nafikiri ipo haja hiyo, Mhe. Mwanasheria Mkuu taarifa ya Serikali kuhusu Mfuko wa Miundombinu. Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu aliyonipa ina mambo ambayo hayajakamilika yanayotokana na ofisi yako.

Sasa ni vizuri basi yakakamilishwe angalau ile *legal notice number* ipatikane, maana hamna ile. Sasa kama vitu hivyo havijakamilika na taarifa yenyewe hata saini haina, kidogo inawezekana wadadisi, na hasa Wanasheria mnaweza mkasema hii taarifa mmeiokota njiani pahala. Kwa hiyo, nafikiri tufanye hivyo.

Kwa kuwa kuna masuala mengine, kwa mfano hapa nimeletewa hiyo *Establishment of the Infrastructure Fund,* kuna *legal notice number,* ndio katika hayo mambo yaliyokuwa hayajakamilika.

Huku mwisho Mhe. Omar Yussuf Mzee alipaswa aweke saini yake ili kuonesha kwamba hiki kitu hakijaokotwa njiani pahala kwa sababu hii ni *notice* rasmi. Sasa nadhani haya mambo yangekamilika yakakaa vizuri. Mwanasheria Mkuu hebu twambie kuhusu kusawazisha hili.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, ni kweli haya ambayo umesema kwamba hii haikutiwa saini na haikutiwa *legal notice* na ina sababu yake.

Sababu yake kwanza haikukamilika, kwa sababu bado Baraza haikuridhia mpaka pale ambapo Baraza itaipitia, kama kuna marekebisho yafanywe, kama kuna mapendekezo yaingizwe mapendekezo yake, ili sasa tunapotoka hapa tunatoka na *document* ambayo imesharidhiwa na Baraza ndio pale sasa Mhe. Waziri anakwenda kutia saini. Na anapotia saini ndio pale tunaitia nambari tunakwenda kuitangaza kwenye Gazeti Rasmi la Serikali. Tutapofanya vyenginevyo itakuwa utaratibu tumeukiuka Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** *Legal notice number* inatiwa baada ya taarifa hiyo kutolewa rasmi Barazani na kupokelewa na Baraza hili, ndio utaratibu wake, *okay*.

Sasa hoja hiyo imekaa sawa, kama hoja imekaa hivyo basi iko sawa.

Waheshimiwa Wajumbe kuhusu kupata hizi *document* nadhani hili lisiwe hoja tukubaliane tusitishe shughuli hii kwa muda kidogo, na moja kwa moja kwa sababu Wajumbe wenyewe ndio sisi hapa hakuna wengine wa kuwasubiri, wachache sana wako nje.

Kama katika kipindi hicho kutakuwa na maoni sasa ya wale Wenyeviti ya kuandika tutarekebisha hii *order paper,* ili ile hati ya Mwenyekiti ya kuwasilisha maoni yaliyoandikwa nayo sasa iwasilishwe.

Na katika kipindi hiki basi, tunapoahirisha kwa muda fulani, sijui kwa muda wa saa ngapi tunahitaji, *two hours?* Hapana! Tusifanye kesho, kwa sababu tuna mtiririko wa mambo mengi.

Hivi sasa tusitishe shughuli zetu tupande hapo juu tukaanze ile shughuli ya marekebisho ya Kanuni, ili tuifanye kazi hiyo, na kwa sababu jambo lenyewe halitachukua muda mkubwa, basi mimi nataka nisitishe shughuli hizi hadi saa 6:00 ili tukamilishe vizuri na kazi hii tutakuja kuimaliza kwa muda uliobaki.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe baada ya matokeo hayo ambayo ni muhimu kwa ajili ya kufanya shughuli hii iende vizuri, angalau iwape nafasi wale Wenyeviti wakipata hii *document* kutayarisha haya maelezo ya Mwenyekiti au

kama itakuwa wanamteua Mjumbe mwengine kwa idhini yao basi wafanye hivyo, tusitishe shughuli zetu hizi hadi saa 6:00 mchana ambapo shughli hii tutakuja kuifanya.

Wakati huo huo lakini tunapanda hapo juu kuanza shughuli ya Kanuni, na shughuli ya Kanuni ilipangwa iwe Kamati ya Uongozi pamoja na Kamati ya Kanuni kama tulivyosema jana.

Kwa hiyo, shughuli tunasitisha hadi saa 6:00 mchana.

*(Saa 3:29 Baraza lilisitishwa kwa muda hadi saa 6:00 mchana)*

*(Saa 6:00 mchana Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe asubuhi tulianza kupokea Hati Mezani kuhusiana na suala zima la kuundwa Mfuko wa Afya wa Wilaya, lakini pia Mfuko wa Miundombinu.

Hati iliwekwa mezani hiyo na baadae tukamuomba Mhe. Waziri wa Fedha aanze kutoa hiyo taarifa juu ya uanzishwaji wa mifuko hiyo na alianza kwa Mfuko wa Afya Wilayani, na kabla hakumaliza kabisa jambo hilo kimsingi alikwishawasilisha lakini ikaja hoja kwamba jambo hili ambalo tulitaka kujua je, hii ni Taarifa ya Serikali au ni Kauli ya Serikali.

Sasa mtazamo wa Serikali ilikuwa ni kwamba tupate mjadala juu ya jambo hili. Kama tupate mjadala wa maoni ya Waheshimiwa Wajumbe basi maana yake iwe ni Taarifa ya Serikali, lakini kama ilikuwa ni Kauli ya Serikali tu, kwa kawaida hiyo inakuwa haijadiliwi na inabidi ije kama ilivyo hapa kwamba ni Kauli ya Serikali.

Sasa tukaona basi jambo lenyewe limeombwa na Wajumbe kupatikane nyaraka (*document)* au waraka unaohusiana na jambo hili, ili Wajumbe waone hiki kitu chenyewe kilichowekewa hati na hatimae kutaka kufanya mjadala ni nini. Kwa hivyo tukaahirisha shughuli zetu mpaka saa sita hii, ili kurekebisha hayo matatizo na hatimae kupata hizo hati zenyewe ambazo zinagaiwa.

Sasa wakati huo huo tukapata nafasi tukenda kwa undani kidogo kuangalia sheria inayoruhusu uanzishwaji wa mifuko ya aina kama hii. Kwa sababu mifuko hii inaanzishwa kwa mujibu wa sheria na kama maelezo alivyoanza kutoa mapema Mhe. Waziri wa Fedha kwamba mifuko hii inaanzishwa kwa madhumuni maalum. Kwa mfano, kama ule wake ni kwa sababu washirika wa maendeleo watasaidia kuweka fedha fulani, lakini na Serikali pia itakuwa imeweka fedha fulani. Lakini

fedha hii washirika wa maendeleo wanaitazamia kwamba itumike kwa ajili ya mambo ya afya. Kwa mfano tukenda kwenye Mfuko wa Afya.

Sasa zikiingizwa kwenye bajeti ya kawaida ya Wizara ya Afya, sasa ile inakuwa kama inaweza wakati mwengine ikafanyiwa *reallocation* ikatumika kwa mambo mengine na washirika wetu wa maendeleo kidogo wanahisi hilo jambo siyo sahihi. Kwa sababu wao haja yao ni kusaidia masuala ya afya Wilayani.
Kwa hivyo, kwa mtazamo wao wakaona basi ingefaa kuanzisha Mfuko, sisi tutatia kwenye Mfuko na nyinyi mutachangia humo Serikali, ili hatimae ifanyiwe kazi hilo suala zima la afya.

Ndivyo itakavyowapa wao nafasi ya kuja kufanya *auditing* (kuchunguza) matumizi ya fedha zile zimetumika vipi. Na ikiingia kwenye upande wa Wizara ya Afya moja kwa moja, aah! wao hawatokuwa na nafasi ili kufanya *auditing*, kwa sababu *auditing* kwa hawa washirika wa maendeleo wanaweza wakaifanya wao kwa kutafuta taasisi ya kufanya *auditing* au wakamuidhinisha *CAG* wetu akafanya kazi hiyo kwa niaba yao na akawapa taarifa juu ya matumizi ya fedha hizo.

Kwa hivyo kilichojitokeza ni kwamba inabidi kwanza tuitambue hii sheria inasema nini juu ya uanzishwaji wa huu Mfuko. Kwa maana hiyo kabla ya kuendelea na jambo lolote, naona Mhe. Mwanasheria Mkuu yupo nimuombe aisome hiyo sheria, tupate uelewa juu ya sheria hasa inataka nini. Tufanye nini sisi kabla hatukuendelea kusema tunajadili au vyenginevyo. Kwa hivyo nichukue nafasi hii kumuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu awasilishe, asome hiyo sheria itueleweshe kile kinachotakiwa na chombo hiki kifanyaje utaratibu wake.

Mhe. Mwanasheria Mkuu karibu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, ninakushukuru. Kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Sheria Na. 12 ya 2005 Sheria ya Fedha kinasema ifuatavyo;

Mhe. Spika, kifungu hicho ni maalum kwa ajili ya kuanzisha mifuko maalum na kinasema:-

11 (1) *The Minister may by order published in the Gazette, establish special funds which shall not form part of the Consolidated Fund; and the receipts, earnings and the accruals of such funds at the end of the financial year shall not be repaid to the Consolidated Fund but shall be retained by the funds for the purposes for which they were established.*

Mhe. Spika, Kifungu kidogo cha pili kinasema:-

(2) *Any order made under subsection (1) of this section shall:-*

*(a)* *state the purpose for which the special fund is being established; and*

*(b)* *identify the Accounting Officer responsible for its operations; and that order shall be tabled before the House of Representatives and shall be subject to annulment by the House of Representatives and shall cease to have effect when so annulled but without prejudice to the making of a further order.*

**Mhe. Spika:** Haya lugha tunayotumia katika Baraza hili hasa ni Kiswahili, hebu tupe kwa Kiswahili kwa kifupi.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, kiujumla madhumuni ya Kifungu cha 11 ya kwamba kinatoa uwezo kwa Mhe. Waziri wa Fedha wa kuanzisha Mfuko maalum na Mhe. Waziri wa Fedha anapoanzisha mifuko hiyo maalum, ile *order* yake ya kuanzishwa kwa hiyo mifuko anatakiwa sasa aiwasilishe mbele ya Baraza la Wawakilishi, ili Wajumbe sasa wa Baraza waione na wairidhie *order* yenyewe.

*Of course* Kifungu kinaendelea kusema Mhe. Spika, kama Wajumbe pia wana uwezo baada ya kuiona hiyo *notice* yenyewe, kama kuna jambo ambalo wanataka waliamue au walikataze kwenye ile *legal notice* wanaweza wakafanya hivyo. Lakini msingi wake ni kwamba inaletwa ile kwa taarifa ya Baraza kama Mhe. Waziri wa Fedha ameshaanzisha huo mfuko.

Madhumuni yake ni kwamba anatakiwa kwanza amtaje mtu ambae atakuwa anashughulikia huo mfuko (Afisa Mas-ul), lakini pia ataje sababu zake za huo Mfuko.

Sasa hayo ndiyo yale ambayo Waheshimiwa Wajumbe wanatakiwa wayatizame. Kwanza je, hiyo *notice* ambayo Mhe. Waziri wa Fedha ameitoa imeeleza nani atakuwa Afisa Mas-ul wake ambaye atakuwa ndiyo dhamana wa kushughulikia hizo fedha na yeye ndiyo atakuwa anaulizwa pale ambapo utakuja kufanyiwa ukaguzi. Lakini nilieleza madhumuni yake ya kuanzishwa huo Mfuko wenyewe ni nini.

Sasa Wajumbe wakiona hayo tayari yameshatimizwa, sasa ni kuridhia tu na ule utaratibu mwengine ukaendelea.

Mhe. Spika, ninakushukuru.

**Mhe. Spika:** Kwa hayo maneno mengine na kwa kifupi ni kwamba Mhe. Waziri wa Fedha ana uwezo kwa mujibu wa Sheria hii moja kwa moja kuanzisha Mfuko. Wajumbe wanataka kujua kama sheria ndiyo inavyotaka hivyo. Je, mifuko hiyo imeshaanzishwa.

Kama imeshaanzishwa sasa Sheria inasema kwamba basi Baraza liarifiwe. Utaratibu wa kuarifiwa ni kwa kuweka mezani tu au vipi, hebu tusaidie na hili ili baadae tumwambie Mhe. Waziri sasa afanye kile ambacho kinamuhusu afanye.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu**: Mhe. Spika, utaratibu wa kuliarifu Baraza ninadhani tunaujua na tunauzowea, kama Mhe. Waziri *history* yake, ukitazama *history* yake ilivyo wanasema hata ukiwasilisha Ofisi ya Katibu inakuwa ile taarifa imeshafika. Ukitizama ile *history* yake na wenzetu wanavyofanya.

Lakini sisi Mhe. Waziri anawasilisha hapa mbele ya Baraza kwa kutoa tu ile taarifa yake kama lile jambo ambalo anatakiwa kufanya kwa mujibu wa sheria amelitimiza. Hiyo ndiyo tafsiri yake Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Kwa maana hiyo sheria inamtaka awasilishe tu jambo la uanzishwaji wa mifuko ambayo tayari kishafanya. Mhe. Waziri karibu hivi utuwasilishie.

Aah! labda niseme kwanza. Sasa Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa hii sheria inavyohitaji hakuna mjadala wowote juu ya jambo hili. Sheria inamtaka Mhe. Waziri awasilishe tu kazi ambayo ameshaifanya kwamba ameanzisha Mfuko wa Miundombinu kwa mfano, aisome hiyo. Akishaisema imekwisha.

Kuna kifungu chengine ambacho sisi Wajumbe wa Baraza kinatupa nafasi, baadae siyo sasa, baada ya nyinyi kwenda kuangalia angalia yale madhumuni yenyewe mukaona mmh! hapa hapajakaa vyema, kujenga hoja hapo baadae *of course* itabidi hoja ifuate utaratibu wake wa kawaida na Baraza halitakuwa hili tena na muda wenyewe haupo. Huko mbele kwenye majaaliwa.

Baraza lingefaa ikafikiria huu Mfuko katika kipengele fulani kukawa na marekebisho fulani, hoja ya Mjumbe juu ya jambo hilo ndiyo itakuja sawazisha hilo. Lakini Sheria kama inavyohitaji kwa sasa aseme tu hapa kwamba nimeanzisha Mfuko huu kwa madhumuni haya.

Kwa hivyo ilivyo hapa hapana mjadala. *Papers* hizo mulizogaiwa kwenu zitakusaidieni kujua madhumuni ya Mfuko ni nini na kitu gani na kila kitu. Ili kama ukipitia baadae ukiona kuna hoja wakati muafaka huko usoni, basi ujenge hiyo hoja na kuja kuomba kwamba Baraza lifikirie namna ya kuweza na

kusawazisha au kurekebisha hayo madhumuni ya Mfuko yenyewe. Hicho ndicho ambacho kinahitajika kukifanya.

Basi ni hayo nije nimkaribishe Mheshimiwa, lakini Mfuko wa Afya, huu siyo tayari kila kimekwisha. Hebu nipate taarifa na hili ili ninamwita kwa ajili ya kitu gani.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Kwa mujibu wa taarifa ambazo tunazo Mfuko huu wa Afya Mhe. Waziri amesha-*sign* tokea tarehe 1 Julai, 2014, mwaka jana. Sasa tunaamini kwamba Mhe. Waziri ameshafuata ule utaratibu ambao unatakiwa ifuatwe kama huu ambao ataufanya kwa Mfuko wa Miundombinu.

**Mhe. Spika:** Na waliokwishakupata *legal lotice,* namba na kila kitu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** *legal notice* yake namba ni 49.

**Mhe. Spika:** Ni namba 49. Haya.

Kwa maana hiyo kazi ya Mfuko wa Afya Wilayani, kazi hiyo ilikwishafanyika. Wajumbe kama mukitaka muone nini kimo zaidi baada ya ufafanuzi huu na kama munataka kujenga hoja hapo baadae mutafute hiyo *legal notice No. 49* mutajua nini kimo na madhumuni yake na kila kitu.

Mukitaka kujenga hoja kwenye majaaliwa huko usoni, huko usoni munaweza mukaijenga hiyo hoja kwa wale ambao wataajaliwa kuwemo humu ndani.

Kwa maana hiyo sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha aje awasilishe mezani na kutoa sababu zake namna alivyoanzisha Mfuko huo wa Miundombinu.

Mhe. Waziri karibu.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha Hati ya Kisheria Na. 85 juu ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Miundombinu kwa dhamira ya kukusanya ada na mapato mbali mbali ambayo yatakayotumika kwa ajili kuendeleza miundombinu yetu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe hiyo kazi ndiyo imekwisha, imeshawasilishwa, mushaarifiwa kwamba Mfuko umeshaanzishwa na taarifa hiyo ndiyo imeshawasilishwa Barazani na haina haja hata kuwauliza kama mumeipokea au laa. Ila munaelewa kwamba sasa hicho kitu kimeshaanzishwa, kama kuna hoja

basi ipitieni hiyo *legal notice* muone nini ambacho munahitaji kurekebisha, mukiona hakuna marekebisho basi munanyamaza kimya. Ninadhani Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amenifahamu.

Baada ya hapo Katibu kuna shughuli nyengine kwa mujibu wa *order paper* yetu ya leo.

**Katibu wa Baraza wa Wawakilishi:** Mhe. Spika, kwa mujibu wa orodha ya shughuli zetu za leo tumemaliza.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi kuwashukuru, tulipata mkanganyiko kidogo wa kisheria na vizuri chombo hichi tukawa makini sana, ili kuhakikisha kwamba kila kitu kinakwenda kwa mujibu wa sheria iliopo ya kufanya jambo hilo. Sasa tumeshaweka mezani taarifa ya uanzishwaji huu Mfuko wa Miundombinu, Mfuko wa Afya Wilayani ulikwishawasilishwa huko nyuma *legal notice* hii ipo wazi kwenu Waheshimiwa Wajumbe kuweza kuangalia kile ambacho munahisi kama kipo kufanya marekebisho ya aina yoyote.

Katibu ananiambia hakuna shughuli nyengine. Kwa hivyo mimi ninadhani moja kwa moja na wala hapa hatuwezi tukatoa hoja kufuatana na mazingira, ila tusitishe shughuli zetu kwa leo. Kwa maana hiyo nichukue nafasi hii kuahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 25/06/2015, saa 3.00 asubuhi. Lakini Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na wale Wajumbe wa Kamati ya Kanuni tunarudi kumalizia kazi ambayo kesho inatakiwa iwasilishwe hapa.

Labda nitoe taarifa zaidi tu kwamba tunasisitizwa, hili ni wajibu wetu. Tunasisitizwa kwamba Wajumbe wote saa tatu iwe tunafika hapa za asubuhi na kutakuwa na shughuli ya *briefing* kesho kuhusiana na kazi ya Kanuni ambayo tunayokwenda kuimaliza sasa hivi, ili tuweze kuja kuipitisha rasmi iwe ni marekebisho ya Kanuni zetu zitakazotumika kwenye Baraza jipya lijalo. Baada ya kuipitisha katika Baraza, *adoption* yaani kuipitisha rasmi inahitaji Baraza letu litimie. Kwa hivyo ni muhimu kama jana mulivyofanya vizuri mno, tukasifiana humu ndani Barazani.(*Makofi*)

Mimi nimepata *message* kutoka kwa wananchi kusifiwa sana kwa kazi nzuri sana muliyoifanya jana na kwa nidhamu kubwa sana tuliyoonesha mahudhurio yetu, kiasi cha kwamba tukapitisha Mswada ule wa Matumizi kwa taratibu zilizopo tukiwa tumejaa humu ndani Wawakilishi wa Baraza hili kutoka Chama cha CCM. (*Makofi*)

Sisi ndiyo tuliwobaki, mlango wala hatujaufunga ule wakitaka watakuja, hawakutaka nyinyi muliopo mufanye hiyo kazi. Maana wananchi hawajatuletea

Wajumbe wengine zaidi ya sisi na wale waliotoka huko nje. Kwa hivyo, tuliokubali kuendelea kufanya kazi tufanye kazi. (*Makofi*)

Hivyo tunaahirisha Kikao hiki lakini tukijua kwamba tunatakiwa sote tuwepo. Mara ya kuahirisha, Kamati ya Uongozi na Wajumbe wale wa Kamati ya Kanuni tunakutana juu kumaliza kazi za Kanuni.

*(Saa 6:26 mchana Kikao kiliahirishwa hadi tarehe 25/06/2015 saa 3:00 asubuhi)*